**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**

**SHULE YA SEKONDARI KEMARONGE**
**S.L.P 176**
**MUGUMU-SERENGETI**

**Simu: +255 684-420 316**
**+255 757-347 452**

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI ..........................................................................................**

**1.0 YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KEMARONGE, KIDATO CHA KWANZA, JANUARI 2021**

Ninafurahi kukujulisha kuwa, mwanao amechaguliwa kujiunga KIDATO CHA KWANZA katika shule yetu ya sekondari KEMARONGE iliyopo kata ya Mosongo katika kijiji cha Kenokwe, kwa mwaka wa masomo 2021. **"HONGERA SANA".**

Shule itafunguliwa mnamo Tarehe 11.01.2021 siku ya Jumatatu. Aidha, Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni siku hiyo tayari kwa kuanza masomo akiwa amekamilisha mahitaji yote anayotakiwa kuwa nayo, kabla ya kuripoti shuleni kama yalivyoainishwa kwenye fomu hii ya maelekezo.

**LUGHA YA MAWASILIANO KWA WANAFUNZI SHULENI NI KINGEREZA TU.**

**"KARIBU SANA"**

..................................

**JUVENALIS J. CHACHA**

**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
KEMARONGE SEC. SCHOOL
P.O.Box 176 MUGUMU
SERENGETI

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### A. SARE YA SHULE

i) Sketi mbili (02) rangi ya **kijivu nyeupe kitambaa kizito cha suti** (Namba moja) zenye marinda ya kawaida kumi na mawili (12) ndefu zinazovuka magoti. Kwa wasichana tu.
ii) Suruali mbili (02) rangi ya **kijivu nyeupe, kitambaa kizito cha suti** (Namba moja), ZISIZOBANA MWILI zenye marinda na mifuko miwili ya kawaida mbele na mmoja nyuma, ziwe na mkunjo chini (turn up). Kwa wavulana tu.
iii) Shati mbili (02) nyeupe zenye mikono mifupi**, aina ya tomato**, ziwe na mfuko mmoja tu mbele upande wa kushoto, Kwa wavulana na wasichana.
iv) Tai ya pundamilia, mistari inayokatisha (kijivu na mieupe). Inapatikana shuleni kwa Tsh 4,000/= tu.
v) T-shirt moja rangi ya blue yenye nembo ya shule ( inapatikana shuleni) kwa Tsh 11,000/= tu
vi) **Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi, jozi mbili**
vii) Soksi jozi mbili aina ya stocking ndefu nyeupe nzito zisizo na alama au misitari yoyote kwa wasichana tu, na soksi jozi mbili nyeusi nzito kwa wavulana tu.
viii) Mkanda mweusi wa ngozi wa kufungia suruali, kwa wavulana tu
ix) Sweta rangi **NYEUSI** isiyokuwa na alama nyingine yeyote. Yenye shingo la "V"
x) Rangi ya hijab (kijuba) nyeupe isiyokuwa na urembo wowote. Kwa waislamu tu.
xi) Track suit ya Blue aina ya Adidas, ya mikono mirefu kwa ajili ya michezo, (Kwa wavulana na wasichana).
xii) Raba za michezo zinazofaa

**MUHIMU:**
Nimeambatanisha kipande cha kitambaa cha suruali/sketi kinachotakiwa, kama utapata shida wasiliana na uongozi wa shule kwa namba hizo hapo juu.

### B. MAHITAJI MENGINE YA LAZIMA KUJA NAYO SHULENI

**i)** **KITI NA MEZA,** vyenye fremu za chuma na top za mbao, kiti kibinuke kidogo nyuma, kumsaidia mwanafunzi kukaa vizuri.

**ii)** Ream moja ya karatasi aina ya Double A kwa ajili ya matumizi shuleni

**iii)** Fyekeo moja (01) pamoja na Jembe moja (01) lenye mpini, kwa wote **(wavulana na wasichana).**

**iv)** Madaftari makubwa (**Counter Books**) Quire 3, tisa (09) au zaidi.

**v)** Kalamu za kutosha rangi ya Blue ama Nyeusi

**vi)** Mkebe wa Hisabati (Mathematical set)/BOFA moja 01.

**vii)** Rula moja pamoja na penseli aina ya HB.

**viii)** Faili moja kwa ajili ya kutunzia taarifa za maendeleo ya mwanafunzi shuleni

**ix)** Kamusi ya Kingereza (**English Dictionary)** moja

**x)** Vitabu mbalimbali vya masomo kadri utakavyoweza.

xi) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

Chacha
..............................
**JUVENALIS J. CHACHA**
**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
KEMARONGE SEC. SCHOOL
P.O.BOX 176 MUGUMU
SERENGETI

## 3.0 SHERIA ZA SHULE

Sheria za shule ni kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa kwa sheria na. 10 ya mwaka 1995. Hivyo basi, mwanafunzi anapaswa kuzifuata bila kukiuka. Ukiukwaji wa sheria za shule kama zilivyooneshwa hapa chini na zingine kwa mujibu wa sheria ya Elimu, utamfanya mwanafunzi **aadhibiwe, asimamishwe masomo ama kufukuzwa shule kabisa.**

**Mwanafunzi anapaswa kuzingatia yafuatayo muda wote awapo shuleni;**

i) Heshima kwa walimu, viongozi,wazazi,wafanyakazi wasio walimu, wanafunzi wenzake na jamii kwa ujumla.
ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ya ndani na nje ya shule kwa mujibu wa ratiba ya shule
iii) Kuwahi shuleni na kushiriki katika shughuli za shule na nyingine atakazopangiwa.
iv) Kuifahamu mipaka ya shule na kuizingatia kikamilifu. Ahakikishe anakuwepo ndani ya mipaka ya shule muda wote wa masomo anaotakiwa kuwa shuleni.
v) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vi) Kuvaa kwa **unadhifu na uadilifu** sare ya shule wakati wote awapo ndani na nje ya mipaka ya shule.
vii) Kuzingatia na kutekeleza ratiba ya shule ipasavyo
viii) Kutunza mali ya umma/shule kwa umakini mkubwa.

**Makosa yafuatayo yatasababisha mwanafunzi kuadhibiwa:**

i) Kutokusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita, kuingia darasani au mahali pengine popote pale.
ii) Kutumia Lugha zisizo na maadili mazuri dhidi ya mwalimu, wanafunzi wenzake au mtu mwingine yeyote Yule.
iii) Kutovaa sare sahihi ya shule kwa unadhifu na maadili mazuri
iv) Kutokushiriki katika kazi zozote anazopewa na mwalimu ama viongozi wa serikali ya wanafunzi shuleni
v) Kufuga ndevu kwa wavulana
vi) Kutotii kengere ama kupuuza mwito wa kiongozi anayemuita
vii) Kutoheshimu Picha za viongozi wa serikali (Rais), Nembo ya taifa, wimbo wa Taifa, Bendera ya Taifa na Fedha za taifa.
viii) Kutokubali na kuheshimu tofauti za kisiasa, kidini na kiutamaduni.
ix) Kutohudhuria vipindi darasani bila taarifa ama ruhusa yeyote
x) Kutohudhuria kazi za mikono, mikutano ya shule, ukaguzi, makongamano, michezo, usafi wa mazingira n.k
xi) Kutokuwahi shuleni, na katika shughuli zozote alizopangiwa kulingana na ratiba ya shule.
xii) Kutokuwa nadhifu kimavazi na usafi wa mwili kiujumla
xiii) Kutoiheshimu mipaka ya shule
xiv) Kuingia ofisi za walimu, maabara, nyumba za walimu na wafanyakazi wengine wa shule bila ruhusa
xv) Ni marufuku kutembelea sehemu zifuatazo;
   a) Vilabu vya pombe
   b) Kumbi za starehe
   c) Nyumba za wageni
xvi) Kucheza kamari ama michezo mingine inayofanana na hiyo, mfano Bonanza.

**Makosa yafuatayo akiyafanya mwanafunzi atafukuzwa shule mara moja:**

i) Wizi
ii) Uasherati, ubakaji na ushoga
iii) Ulevi, uvutaji bangi na matumizi ya madawa ya kulevya ikiwemo sigara n.k
iv) Kupiga au kupigana shuleni
v) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule na umma kwa ujumla
vi) Kudharau bendera ama wimbo wa taifa
vii) Kupata ama kusababisha mimba
viii) Kutoa ama kushiriki katika utoaji wa mimba
ix) Kuoa ama kuolewa
x) Kugoma, kuchochea ama kuongoza mgomo au kushiriki katika kuvuruga amani na usalama wa shule kwa namna yeyote ile.
xi) Kukataa adhabu kwa makusudi
xii) Kumiliki ama kutumia simu shuleni
xiii) Kuwatesa ama kuwanyanyasa wanafunzi wenzake shuleni na hata nje ya shule.

.......................

**JUVENALIS J.CHACHA**
**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
KEMARONGE SEC. SCHOOL
P.O.BOX 176 MUGUMU
SERENGETI

## 4.0 USAJILI

Mwanafunzi atasajiliwa siku ya kuripoti shuleni kama ilivyoelekezwa kwenye fomu hii hapo juu, Usajili wote utafanyika **Ofisi Ya Mkuu Wa Shule**. Mwanafunzi anatakiwa kukabidhi fomu ya uthibitisho wa mwanafunzi na mzazi/mlezi ikiwa imeambatanishwa na fomu ya uthibitisho wa Daktari (**medical examination form**) kuhusu afya ya mwanafunzi zikiwa zimejazwa na kuthibitishwa na wahusika.

**"KUMBUKA":**

Fomu ya uthibitisho wa Daktari, lazima ijazwe na daktari baada ya kumpima mwanafunzi na kujua hali yake ya kiafya, kama maelekezo yalivyoelekeza kwenye fomu hiyo iliyoambatanishwa nyuma.

Fomu hiyo ya uthibitisho wa mwanafunzi na mzazi/mlezi imeambatanishwa nyuma ya fomu hii, hivyo ijazwe kwa ufasaha na wazazi/walezi wote wanaohusika pamoja na mwanafunzi mwenyewe.

Nakutakia maandalizi mema ya mwanao kujiunga na shule hii ya sekondari
**KEMARONGE.**

**...................."ELIMU NI URITHI"......................**

**"KARIBU SANA"**

..............................
JUVENALIS J. CHACHA
**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
KEMARONGE SEC. SCHOOL
P.O.Box 176 MUGUMU
SERENGETI

# SHULE YA SEKONDARI KEMARONGE
## FOMU YA UTHIBITISHO/AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI

**SEHEMU A: TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

Jina la mwanafunzi…………………………..……….. Kidato cha ………… Mwaka……….
Shule ya msingi niliyosoma ……………………………… iliyoko kata ya ………………………

**SEHEMU B: TAARIFA ZA WAZAZI /WALEZI:-**

i. Jina la Baba ……………………………anaishi kijiji……………… Kata………..……

   Kazi yake ……………………………. anwani yake …………….. simu ………………

ii. Jina la Mama ………………………… anaishi kijiji …………….. Kata ………………

   Kazi yake ……………………………. anwani yake …………….. simu ………………

iii. Jina la ndugu …………………………… anaishi kijiji …………….. kata ………………

   Kazi yake ……………………………. anwani yake …………….. simu ………………

**SEHEMU C : TAMKO LA MWANAFUNZI MWENYEWE**

Mimi ……………………………………………….. nakiri kuwa, nimezisoma vema na kuzielewa ipasavyo sgeria, kanuni na taratibu za shule na kwamba naahidi:-

Kuzifuata sheria, kanuni na taratibu za shule kama zinavyoelekeza na natambua bila shaka yoyote kuwa sheria,kanuni na taratibu zote za shule zimewekwa kwa lengo la kunisiadia mimi kinidhamu na kitaaluma pia.
Kwenda kinyume na jinsi sheria, kanuni na taratibu za shule zinavyosema ni kosa na nitakuw tayari kwa hatua stahiki za kinidhamu zitakazochukuliwa dhidi yangu kwa lengo la kunirekebisha

## SHULE YA SEKONDARI KEMARONGE

**BOX 176, MUGUMU – SERENGETI**

**SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

To the Medical Officer

………………………..

………………………..

Name of the student ………………………………………….. Form …………Year…………

Dear Doctor,

May you please examine the above mentioned student to confirm his/her fitness to undertaking further studies?

1.Urine ………………………………………………. 2. Stool ……………..……………………….…

3.Physical fitness……………………… 4. VD……………… 5. Tuberculosis…………………......

**A. (i) PRELIMINARY INFORMATION ( By the student before the Doctor)**

| NO. | DISEASE | YES/NO | NO. | DISEASE | YES/NO |
|---|---|---|---|---|---|
| 01 | Tuberculosis | | 10 | Epilepsy | |
| 02 | Pneumonia | | 11 | Ear, nose and trout | |
| 03 | Asthma | | 12 | Skin disorder disease | |
| 04 | Heart trouble | | 13 | Anemia | |
| 05 | Recurrent indigestion | | 14 | Operation (s) | |
| 06 | Jaundice | | 15 | Serious accident | |
| 07 | Dysentery | | 16 | Malaria | |
| 08 | Kidney and urinary trouble | | 17 | Stomach trouble | |
| 09 | Nervous breakdown | | 18 | Eye disorder | |

**B. MEDICAL EXAMINATION REPORT AND DOCTOR'S COMMENTS**

a) Weight
b) Heart beat
c) Vision etc.

**C. MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above and consider that he/she is fit/unfit to undergo further studies.

DOCTORS' NAME AND SIGNATURE ………………………………………………………..…

DATE AND OFFICIAL STAMP ……………………………………………………………….